**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**DAR ES SALAAM**

**MAREJEO NA. 240 YA MWAKA 2020**

**KATI YA**

**MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI**

**WA MAZINGIRA DAR ES SALAAM ................................ MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**GEORGE MAPUNDA ................................................ MJIBU MAOMBI 1**

**WEMA ABDALLAH ................................................... MJIBU MAOMBI 2**

# **HUKUMU**

**S. M. MAGHIMBI, J.**

Katika shauri hili mleta maombi anaiomba Mahakama ifanye marejeo ya maamuzi yaliyotolewa na Mhe. Mohamed Gwae, wakati huo akiwa Msajili wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi. Uamuzi huo ulitolewa mnamo tarehe 23/10/2012 kuhusiana na maamuzi ya Mahakama hii katika mgogoro wa Kazi No. 92 wa mwaka 2007. Maombi haya yameletwa chini ya kanuni ya 24 (1) 24 (2)(a) (b) (c) (d) (e) (f) na 24 (3) (a) (b) (c) (d) na kanuni 28 (1) (a) (b) (c) (d) (e) na kanuni ya 55 (2) ya Kanuni za Mahakama ya Kazi, Tangazo la Serikali Namba 106 la mwaka 2007 (itajulikana kama 'Kanuni za Mahakama ya Kazi'), pamoja na kifungu cha 94 (1) (f) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, [Sura ya 366 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2019] (itajulikana kama

"Sheria ya Ajira"). Maombi haya yameambatanishwa na kiapo kilichoapwa na Bi. Bernadetha Hassan Mkandya, Afisa Sheria Mwandamizi wa mleta maombi, kiapo ambacho kimeapwa siku ya tarehe 25 mwezi Juni, mwaka 2020. Kwa upande wake wajibu maombi walipinga maombi haya kwa kuleta kiapo kinzani cha pamoja kilichoapwa tarehe 06 mwezi Agosti, 2020 huku wakiomba Mahakama hii kuyatupilia mbali maombi ya waleta maombi.

Kwa kifupi mgogoro huu umetokana na chimbuko lifuatalo; wajibu maombi waliajiriwa na mleta maombi tokea kipindi ambacho mleta maombi alijulikana kama shirika la maji DAWASCO, ajira hiyo ilikuws katika nafasi ya ulinzi. Wakiwa kazini, mnamo tarehe 06/03/2003 walituhumiwa kwa kuomba na kupokea rushwa. Shauri lao lilifikishwa katika mahakama ya wilaya ya Bagamoyo na walikutwa na hatia na kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela. Wajibu maombi hao hawakuridhika na maamuzi hayo hivyo walikata rufaa katika Mahakama Kuu ambapo waliachiwa huru mnamo mwaka 2006. Baada ya kuachiwa huru waleta maombi ili kuweza kurejea kwa mwajiri wao ili kuweza kuendelea na ajira zao lakini juhudi zao hazikuwa na mafanikio.

Wakati huo huo, baada ya kushindwa kuendesha shughuli zake DAWASCO iliwekwa chini ya kampuni iitwayo CITY WATER SERVICES

ambapo ajira za wajibu maombi zilihamishiwa huko pia. Lakini pia kampuni ya CITY WATER SERVICES nayo haikuweza kufanikisha majukumu hayo na baada ya kushindwa kuendesha shighuli zake vizuri, lilianzishwa Mamlaka ya Maji na Maji Taka DAWASA ambaye ndiye mleta maombi katika shauri hili. Hivyo walalamikaji baada ya kuachiwa huru walirejea kwa DAWASA ili waweze kurejeshwa kazini lakini juhudi zao hazikufanikiwa kwakuwa DAWASA alikanusha vikali kuwa wajibu maombi sio wafanyakazi wake hivyo aliwashauri warejee kwa mwajiri wao wa zamani kwa hatua zaidi. Baada ya kutopatikana suluhu, mgogoro kati ya wadaawa ulifikishwa Mahakama ya Kazi (kipindi hich ikiitw Industrial Court) na kusajiliwa kama Mgogoro Na. 92 wa mwaka 2007.

Baada ya kusikiliza shauri hilo kati ya pande zote mbili, Mahakam hii, chini ya Mh. I.A. Mtinginjola, Kaimu Naibu Mwenyekiti , alitoa amri akieleza yafuatayo:

> *"Mahakama hii inaona mgogoro huu ulileta ukiwa na sababu za msingi na ninaona umeshinda kwa asilimia mia, naamuru walalamikaji kulipwa tofauti ya nusu mishahara kuanzia pale DAWASA alipowakabidhi kwa CITY WATER kwani yeye tofauti*

*ameshawalipa tayari hadi pale walipofungwa ambapo ndipo walikosa kabisa hata ile nusu mshahara,*

*pili kuwalipa mishahara kamili kwa muda wote hadi pale itakapo waachisha kisheria (Malipo haya yafuate mabadiliko yote ya mishahara yao). Na wao DAWASCO watawadai CITY WATER SERVICES on their own time, (Malipo haya yafuate mabadiliko yote ya mishahara yao)., hivyo kwakuwa kutofanya kazi haikuwa kosa la walalamikaji kwani wameonekana kama "Inoccent" mbele ya macho ya sheria.*

*Tatu kwa wao kuonekana hawana hatia, basi maamuzi ya kufukuzwa kazi yote ni batili na ninaamuru warudishwe kazini mpaka pale mwajiri atakapowaachisha kisheria ...."*

Kufuatia maamuzi hayo ya mahakama kama ilivyoamriwa hapo juu, na pia kwakuwa DAWASA kutokana na sababu za kiutendaji aliwapunguza kazi kitengo chote cha ulinzi walichokuwa wakifanya kazi wajibu maombi, aliamua kuwaachisha kazi rasmi wajibu maombi mnamo tarehe 10/05/2010 na kila mmoja alilipwa stahiki zifuatazo:-

i. Mshahara wa mwezi mmoja badala ya notisi.
ii. Michango ya NSSF /PPF kutegemea na mfuko aliokuwa anachangia.

iii. Mshahara wa miezi kumi na mbili

iv. Malipo ya mshahara kuanzia Mei 2005 hadi Mei 2010, miezi 23 mshahara wa zamani na miezi 37 mshahara mpya.

v. Malipo ya kiinua mgongo kufuatana na sheria.

vi. Malipo ya mizigo na nauli kutoka Bagamoyo hadi Dar es salaam (ililipwa kwa mleta maombi wa kwanza tu

vii. Kupatiwa cheti cha utumishi.

Baada ya kutoridhika na malipo yaliyoainishwa hapo juu, wajibu maombi walifungua maombi ya kukazia hukumu wakiiomba Mahakama iwalipe mafao sawa na watumishi waliopunguzwa kazi kutokana na mabadiliko ya kimfumo (redundancy). Katika maombi yao ya ukaziaji hukumu wajibu maombi waliomba mafao yafuatayo:-

| No. | Items | George | Wema |
|---|---|---|---|
| 1. | Unlawful termination | 2,508,000/= | 2,508,000/= |
| 2. | Month Notice | 214,000/= | 214,000/= |
| 3. | Golden hand shake | 10,272,000/= | 10,272,000/= |
| 4. | Travelling costs on repatriation | 300,000/= | 300,000/= |
| 5. | Travelling expenses (luggage) | 2,250,000/= | 2,250,000/= |
| 6. | Leave due but not taken | 2,250,000/= | 2,250,000/= |
| 7. | Leave allowance | 1,478,000/= | 1,478,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8. | PPF contributions | 15,503,640/= | 15,503,640/= |
| 9. | Compensation for PPF termination | 20,000,000/= | 20,000,000/= |
| 10. | 2 years salary | 2,461,600/= | 2,461,600/= |
| 11. | 36 months salary compensation for premature | 11,340,000/= | 11,340,000/= |
| 12. | **Termination of employment** | **67,307,000/=** | **38,247,240/=** |
| 13. | **Corrected Sum/Total** | **67,307,000/=** | **70,033,040/=** |

Mleta maombi alipinga vikali ukaziaji wa mafao hayo hivyo pande zote mbili zilisikilizwa na Mh. Msajili aliamuru kuwa kwakuwa wajibu maombi tayari wameshalipwa mafao yaliyoainishwa hapo awali basi wanastahili pia walipwe mafao yaliyoainishwa katika kipengele cha 3 (mkono wa heri/golden hand shake), mafao ya kipengele cha 6 (posho za likizo/leave pay due but not taken) Pamoja na mafao ya kipengele cha 11 (fidia ya upunguzwaji kazi/36 and 48 salary compensation for retrenchment for 1st and 2nd respectively). Baada ya kutoridhishwa na maamuzi hayo ya Msajili ndipo mleta maombi ameleta maomba haya kwa kueleza na sababu zifuatazo:-

i. Kwamba, Mheshimiwa Msajili hakujielekeza sawa kisheria na kimantiki kwamba wajibu maombi walistahili kulipwa mkono wa

heri kama ilivyotumika kwenye mchakato wa kuwapunguza wafanyakazi mwezi Januari 2007 ilihali wajibu maombi hawakuwa miongoni mwa wafanyakazi waliopunguzwa kazini hata hivyo kiasi cha fedhwa wanachodai hakijawahi kutolewa na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ('itajulikana kama Tume').

ii. Kwama, Mheshimiwa Msajili hakujielekeza sawasawa kisheria na kimantiki kwa kuamua kwamba wajibu maombi walistahili kulipwa likizo ili hali wajibu maombi hawakuwepo kazini lakini pia kiasi hicho cha pesa hakikufanyiwa ukokotozi kwenye Tume.

iii. Kwamba, Mheshimiwa Msajili hakujielekeza sawasawa kisheria na kimantiki kwa kuamua kuwa wajibu maombiwalistahili kulipwa mishahara ya miezi 36 na 48 kama fidia ya kupunguzwa kazini, kwa kumaanisha kwamba ni mkono wa kwaheri, lakini pia haikufanyiwa ukokotozi kwenye Tuzo ya Tume.

iv. Kwamba, Mheshimiwa Msajili hakujielekeza sawasawa kisheria na kimantiki kwa kuamua kwamba wajibu maombi walistahili kulipwa fidia na alichukulia kesi hiyo kama mpya.

v. Kwamba, Mheshimiwa Msajili hakujielekeza sawasawa kisheria na kimantiki kwa kuamua wajibu maombi wanastahili kulipwa kama mkataba wa hali bora unavyosema ilihali wakati kipindi cha

upunguzaji wa watumishi mkataba huu ulikuwa umeisha mda wake mpaka kufikia Julai 2008.

vi. Kwamba, Mheshimiwa Msajili hakujielekeza sawasawa kisheria na kimantiki kwa kukokotoa kiasi cha fedha kwa mahesabu yaliyofanywa na wajibu maombi ilihali kiasi hicho cha fedha hakipo kwenye Tuzo hiyo ya Tume.

Shauri hili liliendeshwa kwa njia ya maandishi. Leta maombi aliwakilishwa na Bwana Amos Enock na Bi. Zakia Selemani wote Mawakili wa Serikali wakati wajibu maombi waliwakilishwa na mjibu maombi wa kwanza kwakuwa mjibu namba mbili alikuwa mgonjwa.

Katika mawasilisho yake, wakili wa mleta maombi aliunganisha sababu ya i, ii, iii, iv na vi. Bi Selemani alieleza kuwa Mheshimiwa Msajili hakujielekeza kisheria kuamua kwamba wajibu maombi walistahili kulipwa kiasi cha shilingi milioni arobaini na tisa laki nne sabini na tisa elfu (49, 479,000/=) kama mkono wa kwaheri, likizo na mishahara ya miezi 36 na 48 kama fidia ya kupunguzwa kazini kwa wajibu maombi. Alieleza kuwa Mheshimiwa Msajili alitakiwa kujielekeza katika kile kilichoamuriwa na sio kuanza kusikiliza kesi na kukokotoa upya.

Wakili Selemani alieleza kuwa mamlaka ya wasajili yameelezwa katika **Order XXI R.21 ya** Sheria ya Mwenendo wa Mashauri Madai, Sura 33

Kama ilivyofanyiwa Marejeo mwaka 2019 ('Sheria ya Mwenendo wa Madai') ambapo katika kifungu hicho msajili hana mamlaka ya kufanya ukokotozi. Alisisitiza kuwa ni takwa la kisheria kuwa msajili wa mahakama kuu hana mamlaka ya kukokotoa kiasi chochote cha fedha kazi yake ni kutekeleza kile ambacho kimeamriwa na mahakama ya chini. Aliongeza kuwa msimamo huo uliamriwa katika kesi ya George Mapunda na Wema Abdallah dhidi ya DAWASCO, Maombi ya Mapitio Na. 01/2014 ambapo iliamuriwa kuwa: -

> *'ni matumaini kwamba kwa nia ya kurahisisha utendaji wa kazi katika sheria za kazi msajili kupewa mamlaka ya kutafsiri au kukokotoa kiasi cha fedha kama utaratibu unavyotaka kwa sasa hivi sio msimamo wa kisheria, msajili hana mamlaka ya kukokotoa kiasi cha fedha, kazi yake kubwa ni kutekeleza kile ambacho kimeamuliwa kwenye mahakama ya chini.'*

Wakili Selemani aliongeza kuwa msimamo huo hapo juu ulielezwa katika kesi ya **Hubert Lyatuu dhidi ya TANESCO**, Maombi ya Mapitio Na. 90/2018, Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, Mwanza. Alisisitiza kuwa kitendo cha Mh. Gwae kusikiliza na kukokotoa kiwango cha fedha ambacho hakijawahi kutolewa na mahakama ya chini ni ukiukwaji wa

sheria na taratibu. Kutokana na hoja hizo aliiomba mahakama itengue maamuzi hayo ya Msajili.

Majibu ya hoja ya walalamikiwa yaliwasilishwa na Wakili Luguwa ambaye katika mawasilisho yake kupinga shauri hili ametumia muda mwingi kuelezea historia ya mgogoro huu ambayo tayari imeelezwa hapo juu. Hivyo sioni sababu ya msingi ya kurudia tena kuelezea historia hiyo. Akijibu hoja ya msingi ya endapo Msajili alijielekeza sawa kisheria katika maamuzi yake, Bwana Luguwa alieleza kuwa Msajili alijielekeza tu katika utekelezaji na wala sio kukukotoa kama ambayo muombaji anadai. Hivyo aliomba maombi haya yatupiliwe mbali.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili mahakama imeona kwamba jambo kuu linalobishaniwa ni kama Mh. Msajili alikuwa na mamlaka ya kufanya maamuzi na kuamuru kama alivyoamua. Ifahamike kuwa hapo awali kabla ya Marekebisho ya Sheria Na. 02 ya mwaka 2020 mamlaka ya Wasajili katika kukazia Tuzo yalikuwa hayako wazi katika sheria za kazi hivyo kwa kupitia kifungu cha 55 cha Sheria ya Mahakama ya Kazi ,mahakama ilitumia vifungu vya ukaziaji hukumu vilivyoainishwa katika Sheria ya Mwenendo wa madai. Ni wazi kuwa maombi haya ya ukaziaji tuzo yalifanywa mnamo mwaka 2010 kabla ya mabadiliko ya sheria iliyoainisha wazi mamlaka wa wasajili. Hata hivyo marekebisho

hayo ya sheria yamefanya marekebisho ya vipengele vichache tu lakini mamlaka ya wasajili katika kukazia hukumu ni yaleyale kama ambavyo yameainishwa katika kifungu(Order) cha XLIII cha Sheria ya mwenendo wa madai ambacho kimeeleza kama ifuatavyo:-

*"1. Subject to any general or special direction of the Chief Justice, the following powers may be exercised by the Registrar or any Deputy or District Registrar of the High Court in any proceeding before the High Court-*

*(a) to appoint and extend the time for filing the written statement of defence, to give leave to file a reply thereto and to appoint and extend the time for filing such reply under Order VIII, rule 1, 11, and 13;*

*(b) to order that a suit be dismissed under Order IX, rules 2, 3 and 5;*

*(c) to make an order or give judgment on admissions under order XII, rule 4;*

*(d) to sign decrees under Order XX, rule 7;*

*(e) to admit, reject or allow the amendment of an application for execution of a decree under Order XXI, rule 15;*

*(f) to issue notice under Order XXI, rule 20;*

*(g) to order that a decree be executed under Order XXI, rule 21;*

*(h) to issue process for execution of a decree under Order XXI, rule 22;*

*(i) to stay execution, restore property, discharge judgment-debtors and require and take security under Order XXI, rule 24;*

*(j) if there is no judge at the place of registry, to issue a notice to show cause and to issue a warrant of arrest under Order XXI, rule 35;*

*(k) if there is no judge at the place of registry, to order attendance, examination and production under Order XXI, rule 40;*

*(l) to order that an agreement, compromise or satisfaction be recorded under Order XXIII, rule 3; and*

*(m) to exercise the powers and duties of a judge or of a magistrate and may pronounce judgements and sign decrees and make orders and transact the business of the High Court or the court of a magistrate."*

Kifungu nukuliwa hapo juu kimeeleza bayana mamlaka ya Wasajili katika kukazia hukumu pamoja na kazi zake nyingine. Kwa sasa, katika Mahakama hii Msajili ana mamlaka ya kukazia tuzo zinazotolewa na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Tume) kwa mujibu wa Kifungu cha 89 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini.

Baada ya kupitia maamuzi ya Mhe Msajili nimeona kuwa hakuna sehemu yoyote ambapo ameamua kuhusu kesi ya msingi kama anavyodai Mleta maombi. Maamuzi yalijikita kwenye stahiki za Wajibu maombi ambao wangetakiwa kulipwa kama ilivyo kwenye maamuzi ya Mahakama hii (Mhe Mtiginjola). Hakuingilia kitu chchote bali ukisoma maamuzi yake yanaendana na kile alichoamua Mhe KN mwenyekiti kwenye shauri la kazi Na. 92/2007 kwahiyo alikuwa tu anathibitisha maagizo wa Mahakama na hakuongeza chochote ambacho hakikuwepo kwenye maamuzi ya msingi. Hivyo basi kwakuwa kilichokuwa kinabishaniwa ni stahiki za Wajibu maombi kwenye tuzo bishaniwa, ilikuwa ni sawa kwa Mhe msajili kufanya maamuzi yale ili kubainisha ni kitu gani kinatakiwa kulipwa na kitu gani hakitakiwi kulipwa.

Baada ya kuona hoja hizo na kile ambacho nimekifanyia uchambuzi na ufafanuzi, Mahakama hii inaona kuwa maombi haya hayana msingi na inayatumbilia mbali. Wadaawa waendelee kukazia tuzo kama

ilivyoamriwa na Mhe Msajili katika kutekeleza maamuzi ya Mhe. Kaimu Naibu Mwenyekiti ya tarehe 03/03/2010. Imeamriwa hivyo.

**Imesainiwa leo Tarehe 16 Mwezi Mei Mwaka 2022**

..................................

**S.M. MAGHIMBI**
**JAJI**